

Bibilia ya watoto
Inaleta



Nuhu na
Mafuriko ya
ajabu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus;
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: M. Maillot; Tammy S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,
lakini bila ya kuuza.



Nuhu alikuwa
mwabudu Mungu.
Watu wote wengine
walimchukia na
kutomtii
Mungu.



Siku moja, Mungu
alisema jambo
la kushtua.



"Nitaiangamiza
dunia hii
iliyoharibika,"

Mungu akamwambia

Nuhu. "Wewe

na

jamii


yako

ndiyo


mtakaookoka."



Mungu alimpa ilani Nuhu kuwa
mafuriko makuu yatatokea
na kufunika ardhi yote.



"Jenga safina," machela
kubwa inayotosha familia
yake na wanyama wengi.
Nuhu aliamrisha.



Mungu alimwuelezea kila
atakacho fanya. Sasa
Nuhu akaanza kazi!





Watu
walimchekelea
Nuhu

alipojaribu
kuwaelezea
sababu yake ya
kujenga safina.





Hata hivyo,
Nuhu aliendelea
kujenga.
Pia

alizidi
kuwaelezea
kumhusu mungu.
Hakuna
aliyemsikiliza.



Nuhu alikuwa na imani kubwa.



Almwuamini
Mungu hata kama
mvua haikuwa
imewahi kunyesha
hapo mbeleni.



Baadaye safina
ilikuwa tayari.




Sasa, wanyama wakaja. Mungu aliwaleta aina saba ya wanyama na wawili wa wengine.



Ndege wakubwa kwa wadogo,
wanyama warefu kwa wafupi
wakaingia ndani ya
safina.



Pengine watu walimtukana Nuhu
alipokuwa akiwaingiza wanyama.
Waliendelea kutenda dhambi.
Hawakutaka kuingia
ndani ya safina.





Mwishowe,
wanyama
wote na ndege
wakawa ndani.





"Njoo
ndani ya
safina,"
Mungu
akamualika
Nuhu. "Wewe
na familia yako."




Nuhu, bibi yake,

wana wake
watatu na
bibi zao
wakaingia
ndani ya safina.

Hapo Mungu akaufunga
mlango wa safina!





Mvua mkubwa
ukaanza kunyesha.
Kulinyesha kwa muda
wa siku arobaini.





Maji yalifurika na
kufunika miji na vijiji.





Wakati
mvua uliisha,
hata milima ilikuwa
imefunikwa. Kila kitu
chenye uhai kilikufa.





Mafuriko yalipozidi
nayo safina
iliendelea kuelea
juu ya maji. Labda
kulikuwa na giza
ndani, labda
hakukuwa na
starehe au hata
kulikuwa kunatisha
ndani ya safina.



Lakini safina
iliwapa Nuhu
na jamii yake
usalama.



Baada ya miezi mitano
ya mafuriko, Mungu
alituma upepo wa
kukausha maji.



Kwa muda, safina
ikaja kutulia juu ya
milima ya Ararat.



Nuhu walikaa ndani ya
safina kwa muda wa siku
arobaini maji ilipozidi
kupungua.



Nuhu akamtuma kunguru na njiwa nje ya safina kupitia dirisha. Alipokosa mahali pa kutua, njiwa akarudi.






Baada ya
wiki, Nuhu
akajaribu
tena.





Wakati huu njiwa
alirudi na jani
bichi la mzeituni
kinywani mwake.





Siku iliyofuata
Nuhu akajua
kuwa ardhi ilikuwa
imekauka kwa vile
njiwa hakumrudia.



Mungu akamwambia Nuhu kuwa
wakati wa kutoka nje ya
safina ulikuwa
umefika.



Pamoja, Nuhu na familia
yake wakawasaidia
wanyama
kutoka.




Nuhu alijawa
shukurani!



Hapo, akatengeneza
madhabahu ambapo

walimwabudu
Mungu ambaye
aliwaokoa
kutokana na
mafuriko.






Mungu
alimpa Nuhu
ahadi ya ajabu.
Kuwa hatawahi
kutuma

mafuriko kuja
kumhukumu
binadamu.





Mungu
akaweka
kumbusho la
ajabu la agano
yake.

Upinde ndio
ulikuwa ishara
ya ahadi hiyo.



Nuhu na familia yake wakapata mwanzo mpya baada ya mafuriko.



Kwa wakati,
vizazi vya Nuhu
wakajaza ardhi
mara nyingine.



Mataifa
yote ya dunia
yalitoka kwa Nuhu
na watoto wake.



Nuhu na Mafuriko ya ajabu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu,
Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 6-10

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu
Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na
anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani
yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya
kwa Mungu:

Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya
dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na
siku moja nitaenda kuwa nawe millele.
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama
mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila
siku! Yohana 3:16

